



TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU WA UFUNDI KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025 UNAOANZA SEPTEMBER 2024

1.0. UTANGULIZI

Mkuu wa Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC) anatangaza nafasi za kujiunga na kozi za Mafunzo ya Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi kwa mwaka wa masomo 2024/2025 unaoanza Septemba, 2024.

1.1 KOZI ZA MAFUNZO

STASHAHADA YA UALIMU WA UFUNDI NA UFUNDI STADI (ORDINARY DIPLOMA IN TECHNICAL AND VOCATIONAL TEACHER EDUCATION)–NTA LEVEL 6

SIFA ZA KIJUUNGA

Muombaji awe na Stashahada ya Ufundi sawa na 'Ordinary Diploma' (NTA Level 6) au sifa linganishi zinazotambulika na Mamlaka za urekebu na ithibati.

MUDA WA MASOMO

Muda wa masomo kwa kozi hii ni Miaka Miwili (Miezi 24).

CHETI CHA WALIMU WASAIDIZI WA UFUNDI STADI (CERTIFICATE OF ASSISTANT VOCATIONAL TEACHER)

SIFA ZA KIJUUNGA

Muombaji wa kozi hii anatakiwa awe na:

- i). Cheti cha Elimu ya Sekondari (CSEE) chenye ufaulu usiopungua masomo mawili, bila kujumuisha masomo ya dini, na
- ii). Cheti cha Ufundi Stadi Ngazi ya 3 (National Vocational Award Level III) au Cheti cha Majaribio ya Ufundi Stadi Daraja la Kwanza (Trade Test Grade One) au sifa linganishi inayotambulika na Mamlaka za urekebu na ithibati.

MUDA WA MASOMO

Muda wa masomo kwa kozi hii ni mwaka mmoja (Miezi 12).

1.2 MFUMO WA UJIFUNZAJI

1.3.1 KUHUDHURIA MAFUNZO YA ANA KWA ANA CHUONI - MVTTTC

1.3.2 KUHUDHURIA MAFUNZO KWA NJIA YA ELIMU MASAFI NA UJIFUNZAJI HURIA (DOEL)

KUPITIA VITUO VIFUATAVYO VYA KANDA:

- i. Kanda ya Kaskazini - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Moshi (VETA Moshi).
- ii. Kanda ya Ziwa - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Mwanza (VETA Mwanza).
- iii. Kanda ya Kati - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dodoma (VETA Dodoma).
- iv. Nyanda za Juu Kusini - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma Cha Mkoa wa Iringa (VETA Iringa).
- v. Kanda ya Dar es Salaam - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Dar es Salaam (VETA Dar es Salaam).
- vi. Kanda ya Magharibi - Chuo Cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Tabora (VETA Tabora).
- vii. Kanda ya Mashariki - Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTTTC).

2.0 ADA ZA MAFUNZO KWA KILA KOZI

Maelezo zaidi kuhusu muundo wa ada yanapatikana katika tovuti ya chuo www.mvttc.ac.tz.

3.0 UTARATIBU WA MAOMBI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO

Maombi ya kujiunga na mafunzo yanafanywa kwa kujaza fomu inayopatikana kutoka tovuti ya VETA: www.veta.go.tz au MVTTTC: www.mvttc.ac.tz kwa gharama ya Shilingi 10,000 tu. Maelezo ya namna ya kupata "Control Number" kwa ajili kulipia fomu yanapatikana kupitia Ofisi ya Uhasibu ya Chuo.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 30 SEPTEMBER, 2024.

**KWA MAELEKEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA
0682 292 094, 0718 142 533, 0673 310 225**

Tangazo hili limetolewa na
Mkuu wa Chuo
Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro,
Tarehe 14 Juni, 2024

S.L.P. 671, 1 Barabara ya Rwegasore, 67181 Boma, Morogoro CBD
Simu:+255 23 2614466, Nukushi: +255 23 2614466,
Barua Pepe: mvttc@veta.go.tz, Tovuti: www.mvttc.ac.tz